مَنْ تَخْتَارُ لِبِنْتِكَ؟

JE,

UNAMCHAGUA NANI

KWA AJILI YA BINT YAKO?

Mtunzi

Sh. Ahmad Bin Mubaarak Al-Mazrui حَفِظَهُ اللهُ

Tarjama

Abu Halima Arafaat Bin Mahmoud

بسم الله الرحمن الرحيم

Ametaja Ibn Abi Ddun-ya katika kitabu chake, kwamba mtu mmoja alimuuliza Al-Hassan Al-Baswriy **-Allaah awarehemu-:**

"إِنَّ عِنْدِي ابْنَةً لِي وَقَدْ خُطِبَتْ إِلَيَّ فَمَنْ أُزَوِّجُهَا؟ قَالَ: زَوِّجْهَا مَنْ يَخَافُ اللَّهَ، فَإِنْ أَحَبَّهَا أَكْرَمَهَا وَإِنْ أَبْغَضَهَا لَمْ يَظْلِمْهَا"

[Nina binti yangu na amechumbiwa kwangu (ameposwa), hivi nimuozeshe nani? Akasema: Muozeshe mtu anayemcha Allaah, kwa sababu akimpenda atamheshimu, na akimchukia hatamdhulumu][1].

Katika athari hii kuna faida nyingi hasa zinazohusu jamii yetu:

Faida Ya Kwanza: Mtu anapotaka kumuozesha binti yake kwa mtu yeyote au kumtafutia mke (kumposea) kijana wake, lazima aombe ushauri na rai kwa watu wa elimu ya Dini, na atahadhari mtu kushauriwa na watu wajinga (wasiojua Dini) na wenye kufuata matamanio ya nafsi zao, kwa sababu kila mmoja katika hao atavutia kwenye linaloafikiana na matamanio yake, basi ni juu yao Mawalii (wasimamizi) wa binti na pia akina mama kuzingatia jambo hili, huenda kwa sababu ya kufuata ushauri mbaya ikawa ni sababu ya kumpoteza binti au kijana wako, kwa kumuozesha mtu ambaye ataharibu maisha yake na kizazi chake!

Faida Ya Pili: Mtu bora anayefaa kuozeshwa ni Mchamungu (anayemuabudu Allaah, na kujichunga na mambo ya haramu), makusudio yake ni mtu aliyekusanya sifa mbili muhimu, Uchamungu na Tabia nzuri, kwa kauli ya Mtume **-swala na salamu zimshukie-:**

[1]- Tazama kitabu: [Al-'Iyaal] (Jz. 4, Uk. 270). Cha Ibn Abi Ddun'ya

"إِذَا أَتَاكُمْ مَنْ تَرْضَوْنَ خُلُقَهُ وَدِينَهُ فَزَوِّجُوهُ، إِلَّا تَفْعَلُوه تَكُنْ فِتْنَةٌ فِي الْأَرْضِ وَفَسَادٌ عَرِيضٌ"

[Atakapokujieni (kuposa) mtu ambaye mnamridhia tabia na dini yake, basi muozesheni, msipofanya hivyo itapatikana fitna katika ardhi na uharibifu mkubwa][2].

Kwanini upatikane uharibifu na fitna kwa kutomuozesha mtu mwenye dini na tabia nzuri?, kwa sababu mtu asiyejua dini hajui haki za mke, na asiyekuwa na tabia nzuri hawezi kuishi nae kwa maelewano mazuri, matokeo yake hupatikana katika ndoa yao magomvi na mifarakano (ya mara kwa mara), ambayo natija yake ni kuachana, jambo ambalo hupelekea kwenye kukosekana malezi bora kwa watoto na familia.

Amesema As-Sha'bi **-Allaah amrehemu-:**

"مَنْ زَوَّجَ فَاسِقًا فَقَدْ قَطَعَ رَحِمَهُ"

[Atakaemuozesha (binti yake mtu) muovu, basi ameukata ukoo wake][3].

Mtu faasiq (muovu) anasababisha kukatika kwa ukoo, kwa sababu ya matangamano mabaya na mke, mpaka itafikia hatua binti haelewani na wazazi wake (baba na mama), na anawachukia kwa sababu ya mume muovu aliyemuoa.

Faida Ya Tatu: Nyumba za wanandoa zina hali nne:

1. Nyumba ambayo hupatikana ndani yake kupendana na kuhurumiana, hii ndio nyumba bora zaidi; mapenzi ni sababu ya kitu kidogo utakiona kikubwa na kichache utakiona kingi,

---

2- Sunan Ibn Maajah (1967).

3- Tazama kitabu: [Al-iyaal[Jz. 1, Uk. 270). Cha Ibn Abi Ddun'ya.

na kwa sababu ya huruma, utaweza kuvumilia kasoro na mapungufu ya mwenzako, na pia kusameheana. Hakika hii ndio nyumba yenye salama daima.

2. Nyumba ambayo hakuna kupendana wala kuhurumiana, nyumba hii ni adhabu ambayo mwisho wake ni kuachana, kwa sababu, vyovyote mke atakavyojitahidi katika kutenda wema na kumhudumia mume wake, mume hawezi kuridhishwa na huduma hizo, kwa sababu hakuna mapenzi. Kama ilivyosema:

وَعَيْنُ الرِّضَا عَنْ كُلِّ عَيْبٍ كَلِيْلَةٌ وَلَكِنَّ عَيْنَ السَّخْطِ تُبْدِي المَسَاوِيَا

Na jicho la kuridhia kwenye kila kasoro halioni

Lakini jicho la kuchukia hudhihirisha mabaya

Katika nyumba hii, kheri yoyote itakayofanywa na mmoja wa wanandoa hao (mume au mke) itakuwa haina thamani kwa mwenzie, na jicho hujifanya chongo halioni wala kuipongeza kheri hiyo, matokeo yake kila mmoja anasubiri kupatikana kosa kwa mwenzie!, nyumba hii imekosa huruma, upendo, na kuvumiliana, mara chache watu hao kudumu katika ndoa yao.

3. Nyumba ambayo wanandoa wanapendana lakini hakuna kuhurumiana, (huenda mtu amevutika na maumbile na uzuri wa mke, kiasi anadhani kama atamuacha hawezi kupata mfano wake, au amependa kabila lake, au ukoo wake, na mke pia, huenda amempenda mume kwa ajili ya pesa, mali, n.k), nyumba hii pia ina kasoro, hata kama wataendelea kuishi lakini kutapatikana dhiki, tabu na pia mmoja kumkejeli mwezie, kiasi ambacho hakuna raha ya ndoa.

4. Nyumba ambazo hupatikana ndani yake kuhurumiana lakini hakuna kupendana, nyumba hii huenda ikadumu pamoja na kukosekana hisia (ya mapenzi), na huenda mapenzi yatakuja endapo mmoja wao atafanya muamala mzuri kwa mwenzie, kwa sababu tabia nzuri inavutia katika upendo, angalia namna khalifa wa pili wa waislamu Omar Ibnil Khatwaab **-Allaah amridhie-**, alivyomjibu mtu ambaye alidhamiria kumpa talaka mke wake, Omar akamuuliza, **kwanini unataka kumuacha mkeo?** Akasema: **kwa sababu simpendi**, Omar akamwambia:

"لَيْسَ كُلُّ البُيُوْتِ تُبْنَى عَلَى الحُبِّ، أَيْنَ الرِّعَايَةُ وَأَيْنَ التَّذَمُّمُ؟"

[Sio nyumba zote zinajengwa kwa upendo, uko wapi muamala mzuri na kumkinga (mkeo) na kutokashifiwa (na watu)?].

Riwaya nyingine imekuja:

[Sio nyumba zote zinajengwa kwa upendo, lakini kuishi pamoja kwa heshima na Uislamu][4].

Kwa hiyo mume Mchamungu, hata ikitokea baina yake na mke wake kutofautiana, kiasi cha kukosekana upendo na furaha katika ndoa yao, basi hatomdhulumu, ataishi nae kwa wema, kwa kumtekelezea haki zake, pia kumvumilia mwenzie na wala hatoi nafasi kwa watu wengine kuanza kumkejeli, kumvunjia heshima na kumkashifu.

Faida Ya Nne: inapasa kwa mawalii (wasimamizi) wa watoto wa kike, wamuogope Allaah kuhusu watoto wao wakike, wakati wowote akijitokeza mtu ambaye anastahiki kuozeshwa (kwa vigezo tulivyotangulia kuvitaja), basi muozesheni, wala walii (msimamizi)

[4]- Tazama kitabu: [Hayaatu Sswahaaba] ()

wa binti asifanye khiyana kwa kumficha binti yake kwamba kuna mtu wa kheri amekuja kuleta posa/kuchumbia, na badala yake anamuozesha mtu ambaye hana vigezo vya dini, ima kwa sababu ya kuangalia mali, kabila, udugu, n.k, matokeo yake anampoteza binti yake kwa sababu ya maslahi yake ya kidunia.

Amesema Ahnaf Bin Qais **-Allaah amrehemu-:**

"أَفْعَى تُحَكِّكُ فِي نَاحِيَةِ بَيْتِي أَحَبُّ إِلَيَّ مِنْ أَيِّمٍ قَدْ رَدَدْتُ عَنْهَا كُفُوءًا"

[Kuishi na nyoka mkubwa anayetoa sauti kando ya nyumba yangu inapendeza zaidi kwangu, kuliko kuishi na binti ambaye nimekataa kumuozesha yeye mtu mwenye kustahiki][(5)].

Anaona ni bora kuishi na nyoka katika nyumba yake, kuliko kuishi na binti ambaye ametokea mtu mwenye tabia nzuri halafu yeye hakuozesha. Huenda watu wengi wasielewe uzito wa maneno haya![(6)].

Wabillaahi Ttaufiiq

Markaz Sheikhil Islaam Ibn Taymiyyah
12/jumaadal Aakhira/1444H – 05/01/2022M.

---

[5]- Tazama kitabu: [Al-iyaal[Jz.1, Uk. 284). Cha Ibn Abi Ddun'ya.

[6]- Watu wengi wameikosa elimu (fiqhi) ya kuchagua mtu wa kumuoa binti yake, pamoja Uislamu ameweka vigezo kuzingatia wakati wa kuchagua mume kama tulivyotangulia kutaja, kwa hiyo anapokuja kwako mtu mwenye vigezo hivyo, kubali ombi lake kwa sababu dini imekuruhusu kufanya hivyo, na wala Allaah hataweka Baraka katika ndoa hiyo, na ikiwa hukuridhika na vigezo mtu mwenye dini na tabia njema), ukamuozesha binti yako kwa mtu ambaye amekosa vigezo, kwa sababu tu ya kufuata mali n.k. na kwa ajili hiyo ndoa nyingi zimekosa mapenzi na furaha yenye kuendelea, bali wapo katika wanaume wamefikia kuwapiga wake zao na hata kuwaua, hayo yote yanatokea kwa sababu mtu hana dini wala tabia nzuri. Tunamuomba Allaah aturuzuku dini na tabia nzuri.